Toleo 59 - Rabi' II 1443 AH / Disemba 2021 M

# UQAB
Jarida la

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Waislamu: Waathiriwa/ Wahanga wa Sera za Ubabe na Uchu wa Ukoloni wa Kimagharibi

**HABARI NA MAONI**
Utawala wa Marekani: Sura Mpya lakini zenye Njama Zilezile

**TOLEO JIPYA**
Je, Teknolojia Mpya ya Kijani ndio Suluhisho la Mgogoro wa Mazingira, au Wembe ni Ule Ule?

**JIBU LA SWALI**
Kuamiliana na Benki za Kiislamu



# Sarafu ya Khilafah ya Dhahabu na Fedha Itamaliza Mfumko wa Bei

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 04/1443 | Jumanne, 04 Rabi' II 1443 H | 09/11/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Waislamu: Waathiriwa/Wahanga wa Sera za Ubabe na Uchu wa Ukoloni wa Kimagharibi.

Baada ya siku kumi na mbili za utekwaji wake, msomi maarufu wa Kiislamu na wakili, Profesa Hassan Nandwa, alipatikana akiwa hai majira ya saa saba usiku 09 Novemba 2021 katika msitu ulioko karibu na mji wa Mwingi. Kama visa vingi vya hapo awali, profesa aliamuriwa kutozungumza kabisa masaibu aliyokumbana nayo vyenginevyo atakiona cha mtema kuni! Kulingana na duru za mashirika ya haki za kibinadamu, mwaku huu zaidi ya watu 133 yasemekana ima kuwa wameuawa au kuchukuliwa na watu hadi mahala pasipojulikana. Tokea mwaka 2007, inakisiwa kwamba zaidi ya watu 1000 wameuwawa au kutojulikana waliko na hatima yao ikibakia kizungumkuti huku serikali haijaonesha angaa msaada wowote ule.

Harakati ya Kiislamu ya Hizb ut-Tahrir Kenya inakashifu na kulaani kwa ukali matendo haya ya kuhofisha na ya kikatili dhidi ya rai waso na nguvu ya kujitetea yanayofanywa na vyombo vya usalama ambavyo kiasili vinatakikana kulinda haki na usalama wa raia. Kwa hakika ukiukwaji huu mkubwa wa haki za kibinadamu wa maafisa wa usalamu ni ishara wazi sifa ya kutojali kwake serikali na kukiuka katiba ya nchi. Watekelezaji wa uhalifu huu bila shaka wanafahamu vyema kwamba hakuna hatua yoyote inayochukuliwa dhidi yao kwani wanapata ulinzi mkubwa. Hata hivyo sisi tunafahamu kwa yakini kwamba Mwenyezi Mungu (swt) sio mwenye kughafilika na wanayoyatenda.

Udhalilifu na unyanyasaji huu unaoshuhudiwa leo ni sehemu tu ya maonevu mengi yanayofanyiwa Waislamu kote duniani chini ya kibandiko cha 'Vita dhidi ya Ugaidi'. Vita hivi vilibuniwa na Wamagharibi kama mbinu ya kusukuma malengo na madhumuni yao; Trojan horse ya kikoloni katika kudhibiti oparesheni za usalama wa mataifa ya ulimwengu wa tatu kumakinisha na kuendeleza zaidi ukoloni wao mambo leo. Kiukweli vita hivi vimewafanya Waislamu wawe wahanga wa ubabe na uchu wa wakoloni. Ni bayana kwamba vita hivi vinaonesha kufilisika kifikra na kisiasa kwa mfumo wa ubepari na fikra zake za kiliberali.

Mateso haya hayotokoma hadi pale Waislamu warudie faradhi yao walioitupa na kuulingania Uislamu kwa lengo la kuregesha maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Khilafah Raashida kwa njia ya Mtume. Njia hiyo haihusishi lolote lile isipokuwa kuingia kwenye mvutano wa kifikra na kisiasa.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi Kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**


Email: info@uqab.or.ke

Afisi ya Habari Wilayah Pakistan

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 22/1443 Jumatatu, 10 Rabi' II 1443 H 15/11/2021 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Sarafu ya Khilafah ya Dhahabu na Fedha Itamaliza Mfumko wa Bei, Unaosababishwa na Uchapishaji Pesa ili Kukidhi Matumizi ya Serikali

Nchini Pakistan, kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2021, rasilimali iliyo katika mzunguko ilipanuka kwa bilioni 2,300, huku amana za benki ziliongezeka kwa bilioni 6,000. Rupia bilioni 8,300 zilifurika ndani ya mfumo katika miaka mitatu tu pekee, huku pato la taifa halikupanda kuendana na ongezeko hilo, kwa kiasi kikubwa likibaki palepale. Matokeo yasiyoepukika yalikuwa ni dhoruba ya mfumko wa bei, kwani nguvu ya ununuzi ya Rupia ilipungua. Bei za bidhaa zote zilipanda sana, na kuwanyima maskini uwezo wa kununua mahitaji ya kimsingi. Tabaka la kati sasa linazama kwenye deni, huku tabaka la chini likilazimika kuomba omba. Hata manufaa ya ongezeko la kawaida la Pato la Taifa yalikuwa kwa kipote maalum, kutokana na mkusanyiko mkubwa wa mali katika mfumo wa kirasilimali. Kwa hivyo, Enyi Watu wenye Nguvu, ni nani atakayejitokeza kuizika maiti hii iliyooza ya mfumo?

Katika Uislamu, hakuna dhana ya sarafu ya karatasi, isiyo na thamani ya ndani. Dinar ya dhahabu ya Khilafah na dirham ya fedha ndizo sarafu za dola. Katika Shariah dinar moja ni gramu 4.25 za dhahabu, huku dirham moja ni gramu 2.975 za fedha. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema, «وَالْوَزْنُ وَزْنُ أَهْلِ مَكَّةَ» **"Na uzani ni uzani wa watu wa Makkah."** (An-Nisai). Sarafu inayotokana na msingi wa dhahabu na fedha huweka nidhamu katika matumizi ya serikali, kwani serikali haiwezi tu kuchapisha sarafu ya karatasi ili kufidia gharama. Kwa hivyo, sarafu thabiti ya dhahabu na fedha ya Khilafah inalinda watu dhidi ya mfumko wa bei wa jumla unaoonekana katika uchumi unaotegemea sarafu ya karatasi, isiyo na thamani ya kindani ambayo hupoteza nguvu yake ya kununua huku zaidi zikiendelea kuchapishwa. Kupungua tu kwa usambazaji au ongezeko la mahitaji ya bidhaa ya mtu binafsi kunaweza kuongeza bei peke yake, huku dola inaweza kuchukua hatua stahiki ili kurekebisha upungufu unaotabirika wa usambazaji, mapema kabisa, kama sehemu ya usimamizi wake wa watu.

Hadi leo, karibu dhahabu na fedha zote zinazozalishwa duniani ziko salama, imara na zinaimarika. Katika karne ya 18 na 19, licha ya kushuka kwa kasi kwa uzalishaji, sarafu ya dhahabu na fedha ilisaidia bei thabiti. Kwa kuwa sarafu ya dhahabu na fedha ni adimu na ya thamani sana, inabaki na uwezo wake wa kuleta utulivu leo. Pia ni sarafu hii ndiyo itakayomaliza utawala haramu ulioanzishwa wa dolari duniani. Amerik hununua kutoka kwa masoko ya dunia kwa pesa zake za karatasi, huku dunia nzima ikilazimika kupata dolari ili kuagiza bidhaa. Pakistan inakabiliwa na dhoruba ya mfumko wa bei, huku uchapishaji wa noti ili kukidhi matumizi ya serikali unadhoofisha sarafu mbele ya dolari. Kisha, kushuka kwa thamani ya Rupia dhidi ya dolari huongeza gharama ya kiasi cha kila uagizaji. Ili kukidhi upungufu wa akiba ya dolari, watawala wa Pakistan huigeukia IMF, ambayo inapanua udhibiti wake wa uchumi wa Pakistan, kupitia mikopo ya riba, iliyo na masharti ya kukandamiza. IMF kisha huusakama uchumi wetu, na kuifanya Pakistan kuwa tegemezi kwa Magharibi na kujinyeyekesha kwake kiuchumi na kisiasa.


Kando na Khilafah kwa Njia ya Utume, ni mfumo upi mwengine unaoweza kumaliza janga la mfumko wa bei duniani? Ikiwa tajiri wa rasilimali kuu za nishati na madini duniani, Khilafah itatumia dinar za dhahabu na dirham za fedha katika biashara ya kimataifa, kurudisha uchumi wa dunia kwenye uwanja thabiti wa sarafu ya dhahabu na fedha. Ulimwengu umeteseka chini ya urasilimali kwa muda mrefu sana na unatazamia kurudi kwa Khilafah pamoja na Uislamu wake, kueneza ustawi. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema, «يَكونُ في آخِرِ الزَّمانِ خَلِيفَةٌ يَقْسِمُ المالَ ولا يَعُدُّهُ» **"Katika zama za mwisho kutakuwepo na Khalifah itaigawanya mali wala haitaiihesabu."** (Muslim). Kando na Hizb ut Tahrir, ni uongozi gani mwengine unaoweza kutawalisha Uislamu kivitendo? Basi watu wenye nguvu nawatoe Nussrah yao kwa Hizb ut Tahrir ili kuiregesha dunia kwenye njia iliyo sawa.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Pakistan**

 Email: info@uqab.or.ke

# HABARI NA MAONI

## Mfumo wa Ubepari Unajali Matajiri na si Wamachinga




**Habari:**

Mnamo tarehe 1/11/2021 Serikali ya Tanzania ilianza zoezi la kuwahamisha maeneo mengine wafanyabiashara ndogondogo nchini maarufu kama "wamachinga" kufuatia maagizo ya Raisi kwa wakuu wa mikoa na wasaidizi wao.

**Maoni:**

Suala la kuhamishwa kwa wamachinga kwenda katika maeneo waliyotengewa siyo geni, kumekuwa na kampeni za aina hiyo katika miaka ya nyuma, kwa mfano ile ya mwaka 2016 iliyowapelekea kuhamishiwa maeneo mapya ya biashara kama vile Kigogo Fresh, Kivule, Ukonga na Tabata Muslim ambayo yalikuwa na uwezo wa kuchukua hadi wamachinga 6,000 lakini zoezi hilo halikufanikiwa.

Mara nyingi kwa kisingizio cha oparesheni kama hizi, Polisi kwa kushirikiana na askari mgambo wa Jiji hujihusisha kukamata, kubomoa vibanda vya biashara na hata kupora kwa kufilisi bidhaa za wamachinga. Vitendo hivi visivyo vya kibinadamu vitaathiri wamachinga ambao ni takribani milioni nne nchi nzima kwa mujibu wa Afisi ya Taifa ya Takwimu, ambapo kati yao 50,000 wanapatikana katika jiji kuu la biashara Dar es Salaam (The East African 15/12/2018)

Ni ukweli usiopingika kuwa suala la wamachinga linahitaji suluhisho bora ili kuepusha matatizo na malalamiko mengi katika miji mikubwa ikiwemo kutozuia njia za watembea kwa miguu nk. Hata hivyo, haya yanahitaji suluhisho lenye dhamira na utashi madhubuti na si maigizo ya kisiasa.

Wamachinga ni watu masikini wenye mitaji midogo sana wanaojaribu kujiajiri katika mfumo wa biashara usio rasmi, baada ya kushindwa kwa serikali kutoa ajira kwao. Kwa miaka takribani mitano iliyopita serikali haijaweza kutoa ajira inavyostahiki, hivyo watu wengi wakiwemo waliomaliza vyuo vikuu hawana ajira.

Ni wazi katika kukabiliana na suala hili, serikali kama zilivyo serikali nyingine za kibepari imeonesha kutowajibika, kiburi na kutojali raia kwani ina wajibu wa kuandaa mazingira bora kwa wamachinga kama inavyofanya kwa makampuni ya kibepari ya kimagharibi ambayo huja kunyonya rasilimali zetu kwa jina la uwekezaji wa kigeni.

Serikali inapaswa kuwasaidia wamachinga kwa kuwapatia maeneo muwafaka na rafiki kibiashara ili wafanye biashara kwa usahali hasa kwa kuzingatia kuwa serikali inakadiriwa kuwa ilikusanya takribani Tsh bilioni 80 (dolari milioni 34.7) kama ushuru kutoka kwa wamachinga kutokana na kuwauzia vitambulisho vya ujasiriamali ambavyo vilikuwa vinatolewa kwa wafanyabiashara ndogondogo wenye mitaji isiyozidi Tsh milioni 4 (dolari 1,900). Ajabu! Mara baada ya kukusanya pesa hizo sasa serikali inawageuka na kuwanyanyasa wamachinga hao!

Katika Uislamu, tofauti na Ubepari, jukumu msingi la serikali ya Kiislamu ya Khilafah ni kuwatumikia watu wote, kwani hiyo ni dhima na amana kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Khalifah-kiongozi wa serikali ya kiulimwengu ya Kiislamu, atabeba majukumu na dhima ya kuwatumikia raia wote bila ubaguzi wa kipato, dini, au rangi zao, nk.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

# HABARI NA MAONI
## Utawala wa Marekani: Sura Mpya lakini zenye Njama Zilezile



**Habari:**

Waziri wa Mambo ya Nje wa Amerika Antony Blinken ataizuru Kenya, Nigeria na Senegal kuanzia Novemba 15-20, akisisitiza umuhimu wa mahusiano yao na washirika wa barani Afrika. (The Star, 12/11/2021).

**Maoni:**

Kwa mara nyingine tena utawala wa Marekani umemtuma mwanadiplomasia wake mkuu barani Afrika kibinafsi baada ya kuzuru Kenya na Nigeria kimtandao mnamo Aprili 2021. Hata hivyo, mara hii Senegal imejumuishwa katika ziara. Ni muhimu kuweza kuzishughulisha akili zetu kwa kujiuliza maswali yafuatayo: 1 –nini kilichonyuma ya ziara hii? 2 – kwa nini kuyazuru mataifa hayo matatu maalumu? 3 – nani anatarajiwa kunufaika zaidi katika ziara hii? 4 – mataifa hayo matatu na Amerika ni washirika katika nini? Maswali hayo manne yatajibika kimakosa lau tutazizingatia taarifa zilizotumwa kwa ummah kupitia vyombo vikuu vya habari ambavyo hupokea malipo ili kupigia debe propaganda za serikali.

Kwa hakika, ziara hii sio chochote bali ni kampeni ya kidiplomasia ya ukoloni mamboleo inayolenga kukazanisha vitanzi katika shingo za watawala vibaraka barani Afrika, ili waendelee kujifunga na mchoro unaoongozwa na mkaazi mpya wa Ikulu ya White House. Mchoro ambao unajumuisha kuyatia pingu mataifa ili kushikamana na mungu aliyefeli wa demokrasia, nidhamu huria ya kijamii, nidhamu ya kiuchumi iliyojikita katika riba na ukandamizaji miongoni mwa maovu mengine yanayo endelea kusababisha majanga yasiyohesabika kwa wanadamu duniani kote. Kwa kuongezea, utawala wa Marekani unakwenda mbio kuzipiku hatua zilizopigwa na utawala wa Uchina barani Afrika.

Mataifa hayo matatu yanacheza dori muhimu katika maeneo yao na barani Afrika kwa ujumla. Kenya ndio kituo cha uchumi wa eneo la Afrika Mashariki na Kati ikiwa haina mshindani. Nigeria ndio yenye uchumi mkubwa na idadi kubwa ya watu barani Afrika. Rais wa Senegal anatarajiwa kuingia katika cheo cha juu katika uongozi wa Muungano wa Afrika (AU). Fauka ya hayo, mataifa hayo matatu yamebakia kuwa watiifu kwa mabwana zao wakoloni ambao ni Uingereza na Ufaransa. Kwa hiyo, Amerika inatambua umuhimu wa mataifa haya na imewekeza juhudi zake ili kuzitoa kutoka kwa washindani wenza wa kikoloni.

Utawala wa Marekani kwa kuwa ndio wenye usemi duniani inatarajiwa kunufaika zaidi kutokana na ziara hiyo. Hata hivyo, mataifa watumwa yatanufaika kutokamana na makombo machache watakayopewa na bwana mkoloni. Amerika itanufaika kupitia utekelezaji wa mikataba mingi itakayotiwa saini nyuma ya pazia na ambayo itayafadhilisha makampuni ya Marekani pasina kuzingatia viwanda vya nchini. Na wakati huo

*Endelea... UK 6*

yakitoa mwanya zaidi kwa taasisi za kifedha za Marekani mfano Benki ya Dunia na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa kuendelea kufanya uharibifu kwa uchumi wa mataifa yaliyosalimu amri.

Amerika na mataifa hayo matatu ni washirika katika kusababisha ufisadi duniani. Kilele cha kiwango cha ufisadi ni wao kuupiga vita Uislamu na Waislamu. Kwa pamoja wameubandikiza Uislamu kuwa ni itikadi kali na Waislamu ni wenye misimamo mikali na magaidi. Hivyo basi, wameamua kuwakandamiza na kuwaua Waislamu kupitia kutunga na kutekeleza sheria na sera dhidi ya ugaidi na misimamo mikali! Kwa pamoja wanaukashifu Uislamu na kuuona kuwa ni wa kikatili na wa kizamani usioweza kutatua changamoto za karne hizi! Alas! Changamoto zilezile ambazo zimetokamana na kutekeleza mfumo batili wa kisekula wa kirasilimali na mataifa yayo hayo!

Kwa kutamatisha, ziara hii haileti matumaini wala ustawi kwa Afrika. Badala yake ni ziara nyingine inayotekelezwa na sura mpya lakini zenye njama zilezile ambayo ni ziara ya kikoloni kuja kutathmini mashamba ya kikoloni yanayomilikiwa na washindani wa Marekani. Lau kutapatikana fursa, basi wajaribu kuwavutia wasimamizi wa shamba la kikoloni kwa vijipesa kwa jina la msaada wa kifedha miongoni mwa vivutio vingine ili kuuhamisha utiifu wao wa kikoloni. Lau hakuna fursa, basi angalau kutafuta japo uungwaji mkono katika kutekeleza ajenda ya Amerika iliyo na sumu ndani ya mataifa yao husika na ng’ambo. Sehemu ya ajenda ikijumuisha kupigana vita vya kiwakala vya Amerika.

Afrika itaendelea kutaabika chini ya mikono ya wakoloni Wamagharibi ambao wanatawala mataifa ya Afrika kupitia watawala vibaraka wa kikoloni. Watawala waovu ambao wanaiba mali za watu binafsi na za ummah na kisha kuzituma ng’ambo ilhali raia wamebakia wanateseka kwa umasikini wa kudumu. Kwa kuongezea, wanakula njama na yale yanayojiita ni mashirika ya Magharibi ambayo hudai kuwasaidia raia; lakini yapo kwa ajili ya kulinda hali iliyoko na kuwahadaa watu. Afrika imezama ndani ya dhiki. Kuchipuza kwa nidhamu mbadala ya uongozi ndio pekee itakayo dhamini kuondoka shidani. Nidhamu mbadala inayochipuza kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt) ni Khilafah kwa njia Utume. Khilafah italeta matumaini na ustawi wa kikweli sio tu kwa Afrika bali kwa dunia jumla. Itakuwa na uwezo wa kuyafanya hayo kupitia utekelezaji wake wa nidhamu tofauti za Kiislamu.

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Mkutano wa 26 Waangusha Jani la Mtini juu ya Ufisadi wa Mfumo wa Kiulimwengu na Kufichua Uongo wa Wale Wanaousimamia

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Zeina As-Samit**

Ni kongamano la 26! Kongamano hilo, ambalo lilifanyika Januari 31, 2021, linamaanisha kuwa kulikuweko na makongamano mengine 25 ya hali ya hewa yaliyotangulia, lakini hayakuleta matokeo ya maana. Kongamano hili lilifanyika na hali za dharura za hewa ziliendelea (kurekodi mafuriko, moto mkubwa, ongezeko la joto duniani, kupungua kwa mazingira asilia, kuenea kwa jangwa, uchafuzi wa mazingira, matetemeko ya ardhi...nk.) kutoa ushuhuda wa kufeli kwa majaribio hayo ya mara kwa mara ya kutatua matatizo haya ya kimazingira ambayo yameenea kwenye sayari hii, na kwamba ulimwengu ulianza kutambua uzito wa hatari ambazo zingeizunguka sayari hii na wale waliomo ndani ya yake katika cha miaka 30 au 40 ijayo.

Kongamano hili, au kama lilivyoitwa, Kongamano la Glasgow, ni fursa kwa viongozi wa dunia kujadili kile ambacho kimetimizwa tangu Kongamano la kihistoria la Paris mnamo 2015 hadi sasa. Kongamano hili lilizingatiwa kuwa muhimu zaidi katika suala la kulazimisha nchi kote ulimwenguni kuchukua hatua za kupunguza ongezeko la joto duniani.

Wajumbe kutoka karibu nchi 200 walikusanyika jijini Glasgow kutafuta njia ya kufikia malengo ya Makubaliano ya Hali ya Hewa ya Paris, ambayo ni kupunguza ongezeko la joto hadi kati ya nyuzi 1.5 na 2, ambapo inahitaji kupunguza uzalishaji unaoongezeka kila mwaka. Nchi 20, ikiwwemo Amerika na Canada, ambazo ni miongoni mwa wafadhili wakuu wa sekta hiyo, zimeahidi kuacha kufadhili miradi ya mafuta ya kisukuku ng'ambo ifikapo mwishoni mwa 2022. Ndiyo, nchi hizi zimeahidi, lakini maelezo ya ahadi hizi hayaeleweki na hakuna ratiba iliyotolewa.

Zaidi ya nchi 40 zimejitolea "kutangaza mabadiliko kutoka kwa makaa ya mawe - aina chafu zaidi ya mafuta ya kisukuku - hadi kwenye nishati safi" katika mpango uliokuzwa na serikali ya Uingereza, na wengi wao wametoa ahadi sawa kama vile Poland na Ufaransa, lakini nchi kubwa zinahusika katika sekta hii, kama vile Australia, China, India, Amerika, Japan na Urusi, hazikuwa miongoni mwa waliotia saini. Je, ni sababu gani ya nchi hizi kupinga kutia saini ili kujifunga na utaratibu huu? Je, sababu kuu ya hilo sio kuhifadhi maslahi yao na kung'ang'ana kupata faida, hata kama ni kwa kuhatarisha wanadamu wote?!

Katika ufunguzi wa kongamano la hali ya hewa, katika wakati ambapo wataalam wa mazingira wanapaza sauti za onyo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres alitoa wito wa kuchukua hatua ili "kuokoa wanadamu," akisema: "Ni wakati sasa wa kusema 'Imetosha'." Na akaendelea, "Inatosha kukiuka maumbile anuwai. Inatosha kujiua wenyewe kwa kaboni. Inatosha kuyachukulia maumbile kama jaa la taka. Inatosha kuchoma na kuchimba na kufukua vina virefu. Tunajichimbia makaburi yetu wenyewe.”

Anamlilia nani? Nchi maskini zinazosubiri misaada, usaidizi na mikopo kutoka nchi hii, benki ile, au muungano ule? Nchi kubwa zinazoongoza ulimwengu na kuchangia zaidi majanga haya ya mazingira, kisha kukwepa jukumu na kutojitolea kutia saini na kuahidi tu pekee, na kuibakisha ahadi hiyo kama wino tu kwenye karatasi? Nani atawaokoa wanadamu na hatari hii na kiongozi wake ni mfumo wa kirasilimali usio na uwezo wa kutafuta suluhu, uliozoea kuakhirisha mambo, kukwepa na kueneza majivu ili dosari zake zisifichuliwe na ufisadi ukadhihirishwa? Wanadamu watatarajiaje suluhisho kutoka kwa wale wanaosababisha matatizo ndani yao? Mnawezaje kusubiri maisha mazuri na kunusurika kutokana na utawala uliojaa ufisadi na wenye kueneza vifo na maangamizi?!

Wanaelezea wasiwasi wao, kwani ni "nafasi ya mwisho" kama ilivyoelezwa na Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson, ambaye alisisitiza kwamba "lazima tuchukue hatua sasa" na alizungumzia mlipuko wa hasira ya wananchi ambayo "haiwezi kuzuiwa" endapo kongamano hilo halitafanikiwa kufikia lengo inalotaka! Kufeli kunakaribia, na kufeli ni anwani pana ya kongamano hili, mithili ya watangulizi wake. Kumekuwepo na makongamano mingi, na kwa kila kongamano linalofanyika, swali linabaki: Je, matatizo ya mazingira yalitatuliwa au yalizidi kuwa magumu zaidi? Na kwa nini?!

Si ajabu kwa nchi za kirasilimali kwamba ahadi zao ni za hazitabiriki na hazieleweki. Nchi hizi ni sawa na vinyonga wanaobadilika rangi kulingana na sehemu zao, hivyo hujitokeza katika makongamano kama hayo, kutafuta suluhu, kueleza kero zao, kusaidia kuziokoa nchi maskini. Kwa kweli, wao ni wanyonyaji damu wa watu, wezi na wakiukaji wa mali na uwezo, kikundi cha unyonyaji, ambacho wasiwasi wao pekee ni kufikia maslahi na kukusanya faida.

***Endelea... UK 8***

Kwa kila kongamano la hali ya hewa linalofanywa, ahadi huwa nyingi - lakini baada ya kongamano hili kupita na mikataba kubaki wino kwenye karatasi tarehe ya kongamano jengine huwasili - washiriki wanasimama kukosoa na kutaka kutekelezwa kwa ahadi za kongamano lililopita ili kupanda matumaini ya uwongo ya utekelezaji wao katika kongamano lao jipya, kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa Laurent Vasos, ambaye aliongoza kongamano la Paris hivyo Kongamano la Glasgow ni "kongamano la kufanya kazi ambalo kwalo tunatekeleza Makubaliano ya Paris." Maneno, maamuzi na ahadi lazima zibadilishwe kuwa vitendo. António Guterres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ameeleza kinachoendelea kuwa ni tahadhari nyekundu kwa wanadamu, akitoa wito kwa viongozi wa dunia kutoa majibu wakati Kongamano lijalo la Dunia la Mabadiliko ya Hali ya Hewa litakapofanyika.

Ijapokuwa matatizo ya kimazingira yanamhusu binadamu kama mtu ili aishi katika mazingira yanayofaa, pingamizi ya Amerika ya kujitolea kufanyia kazi kukabiliana na matatizo hayo, haswa ongezeko la joto duniani, linafichua sera yake mbovu. Je, viwanda hivi ni viwanda vyao wenyewe au vilikuwa katika maeneo mengine kwa njia ya utandawazi, jambo ambalo litapelekea kufungwa au kubadilisha baadhi ya viwanda, jambo ambalo litakuwa na athari mbaya na kupunguza faida ya mali ya watengenezaji, jambo ambalo linapingana na thamani ya kimada yaani juu ya ngazi ya maadili yote kwao... Amerika inakataa kutii yale yaliyoamuliwa katika kongamano hilo, hata kama watu watakosa hewa na kuangamia, au uchafuzi wa mazingira kuongezeka na kuenea, yote hayo hayana thamani maadamu thamani ya kimada hupatikana. Imeshughulikia hali kama hizi hapo awali, kwani hiyo - ambayo ni dola kuu - ilivipa (vita dhidi ya ugaidi) maelezo maalum na fahamu maalum na ya kipekee, na hii hapa inatoa maelezo yayo hayo kwa uchafuzi wa mazingira. Maadamu uchafuzi huu wa mazingira unahuisha kiwanda chake na kuhudumia maslahi yake, unakubalika na ni wa kupongezwa, lakini ukiwa ni kinyume na kile anachokiona na anachokitaka, ni wa kulaumiwa, kukataliwa, na unadhuru mazingira, unadhuru wanadamu.

Ni kongamano litakalofichua tena ahadi na viapo vya uongo vya viongozi wa dunia za kupunguza mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake; kutokana na kupanda kwa viwango vya bahari, hali mbaya ya hewa, na kadhalika. Ni kongamano ambalo halitakuwa bora zaidi kuliko makongamano yaliyolitangulia, na kuibuka kwa maelfu ya wanaharakati na mwaliko wa waandaaji wa vuguvugu la kimataifa "Fridays for Future" - katika jiji hilo la Scotland ambako kongamano hili linafanyika - ili tu kushinikiza viongozi na kupinga ucheleweshaji wao katika kuchukua hatua zinazofaa kudhibiti mabadiliko ya hali ya hewa, wanaahidi kwamba watakutana. Hawaamini na kutoa ahadi na hawatimizi, na kusisitiza kwamba kongamano hili, kama watangulizi wake, halitazaa matunda.

Tatizo la mazingira, kama matatizo mengine yanayowazonga wanadamu; linazidi kuwa baya na kuongezeka, na mfumo wa kimataifa umeshindwa kulitatua, kwa hivyo unaahidi na hautimizi na kuwasilisha maagano na hauyatekelezi, na masharti ya makubaliano na wajibu yanabaki kuwa wino kwenye karatasi yasiyokuwa na uhalisia, na wanadamu wanaendelea kuteseka kutokana na ulafi wa mfumo fisadi wa kirasilimali uliofilisika ambao unaweza tu kuchukua hatua zinazoleta manufaa, hata kama hilo litasababisha kutokomeza zaidi wanadamu. Utawala mbovu, unaosababisha ufisadi, mauaji unaoeneza uvundo wa kifo kila mahali, unaeneza ufisadi bara na baharini na kuleta uharibifu kwa wanadamu, miti na hata mawe.

**[ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ لِيُذِيقَهُم بَعْضَ الَّذِي عَمِلُوالَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ]**

**"Ufisadi umedhihiri bara na baharini kwa iliyo yafanya mikono ya watu, ili Mwenyezi Mungu awaonyeshe baadhi ya waliyo yatenda. Huenda wakarejea kwa kutubu."** [TMQ Ar-Rum: 41]

**#أزمة_البيئة #EnvironmentalCrisis**

# Je, Teknolojia Mpya ya Kijani ndio Suluhisho la Mgogoro wa Mazingira, au Wembe ni Ule Ule?

Wakati Rais wa Amerika Joe Biden alipokuwa kwenye kampeni mnamo 2020, alisema, "Mabadiliko ya hali ya hewa ndio tishio lililopo kwa wanadamu. Ikiwa hayataangaliwa, yataioka sayari hii. Hii sio chuku. Ni ukweli. Na tuna wajibu wa kimaadili." Baada ya kuchaguliwa, ameendelea kushinikiza wazo la kupanua matumizi ya teknolojia ya kijani kwa kuidhinisha Sheria yake ya 'Build Back Better', mpango wa $ 2 trilioni ambao unawekeza katika nishati safi katika sekta ya usafiri, umeme na ujenzi, kupunguza utoaji wa mafuta ya fossil na kuboresha miundombinu.

Baada ya miongo kadhaa ya kuahidiwa kwamba serikali za ulimwengu wa kwanza zitafanya kazi pamoja kupunguza utoaji wa gesi chafuzi, kuunda nishati safi, maji safi, nk, itakuwa kama Greta Thunberg alivyosema hivi majuzi, "Blah, blah, blah," zaidi, kutoka kwa viongozi wa ulimwengu wenye nguvu? Ukweli wa mambo ni kwamba mfumo wa ulimwengu uliopo sasa umeegemezwa juu ya Urasilimali na mfumo wa kirasilimali haukuundwa kufanya kazi kwa manufaa makubwa zaidi ya maisha ya mwanadamu, achilia mbali kufanya kazi ya kulinda mazingira. Urasilimali hauangalii kile ambacho ni cha manufaa kwa wanadamu na mazingira, lakini kile kinachotoa manufaa zaidi ya kifedha kwa serikali, makampuni na kwa Wakurugenzi Wakuu Watendaji na wanasiasa ambao wanalipwa kutunga sheria ambazo ni kwa maslahi yao bora.

Sera za mazingira za urasilimali zimesababisha ukosefu wa usawa wa kushangaza ulimwenguni; upande mmoja kuna matumizi ya kupindukia na ubadhirifu na upande mwingine kuna kunyimwa na unyonyaji. Matumizi ya kupita kiasi yanachochewa na kuzalisha bidhaa za bei ya chini zinazotokana na unyonyaji wa maliasili na vibarua nafuu katika ulimwengu unaoendelea. Unyonyaji unaounyenyekesha ulimwengu unaoendelea kwa mzunguko mbaya wa mizozo na machafuko. Njaa, umaskini, kuhama, uharibifu wa maisha na mali yanayosababishwa na wanadamu katika ulimwengu unaoendelea ni giza tororo la mfumo wa Kirasilimali. Unaiba rasilimali kutoka kwa nchi, bila shaka, ukiwemo ulimwengu wa Kiislamu. Unawaacha watu katika umaskini hohe hahe wakiwa hawana hata punje mchele kama chakula, choo cha kibinafsi cha kutumia, maji safi ya kunywa, unatuma kiasi kikubwa cha nguo kuukuu na vitambaa kama "hisani" na kuviangusha viwanda vyao wenyewe vya nguo kwa sababu ya gharama ya chini, lakini pia unasababisha tani za taka na uchafuzi wa mazingira.

Uhalisia ulipo uwanjani haulingani na ahadi zote zilizotolewa na wanasiasa wa Kimagharibi bila kujali ni sheria na matendo gani waliyopitisha huko nyuma, au wanapanga kupitisha katika siku zijazo kwa sababu haziendani na sifa ya kimsingi ya Urasilimali; kupata faida kwa wachache kwa gharama ya wengi. Hakuna motisha kwa serikali za Magharibi kushughulikia tatizo hili la kimataifa na ni dhahiri kwa sababu hawawezi hata kulishughulikia ndani ya nchi isipokuwa kuleta suluhisho la viraka. Suluhisho la viraka ambalo linahusisha zaidi kuweka mzigo kwa mtu binafsi. Kwa mfano, nchini Amerika, wao huongeza gharama za huduma ili kufadhili mabadiliko ya miundombinu ambayo kampuni binafsi inahitaji kufanya, kuongeza kodi, kuhimiza ununuzi wa paneli za jua za gharama ya juu, kununua gari linaloendeshwa kwa umeme, kununua vifaa vinavyotumia nishati, au kuchukua usafiri wa umma, ambao kwa kweli ni wa kuchukiza kwani miundombinu ya usafiri wa umma ni duni kando na miji mikuu michache. Sasa, ikiwa mabadiliko haya hayawezi kutokea bila ya kuyaweka mabegani mwa watu wa nchi za Magharibi, yatafanya kazi vipi kwa wale wanaoishi katika ulimwengu unaoendelea? Je, paneli za jua, mitambo ya upepo, na magari ya umeme yana manufaa gani kwa watu ambao hawawezi kukidhi mahitaji yao ya kimsingi na hawana usalama? Yatasaidia nini kwa dada zetu kote ulimwenguni ambao hawawezi kulisha watoto wao, au kuwapeleka shule? Je, watawasaidia nini watoto wao wanaougua magonjwa yanayoweza kuzuilika kwa sababu ya maji taka yanayomwagika ndani njia za maji safi, au kufa kwa njaa?

Mgogoro huu wa kimazingira unaweza tu kutatuliwa kupitia utabikishaji wa mfumo wa Kiislamu. Mfumo ambao hutatua matatizo kwa kuzingatia maadili ya kiroho, ya kiutu ya kimaadili na ya kimada. Kwa hivyo, kanuni ya kimada haifadhilishwi juu ya maadili mengine na hakuna yanayopuuzwa kwa faida ya mengine. Ni mfumo ambao msingi wake ni sheria zilizotolewa na Muumba wa mbingu na ardhi. Mfumo ambao utahakikisha kwamba mahitaji yote yanatimizwa bila kuweka mzigo wa kifedha mabegani mwa watu, au kusababisha uharibifu wa mazingira.

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ

**"Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote."** [Al-Anbiyaa': 107]

**#أزمة_البيئة #EnvironmentalCrisis**

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Sarah Mohammed – Amerika**

# Kuamiliana na Benki za Kiislamu




**Swali:**

Assalamu Alaikum wa Rahamtullahi wa Barakaatuh.

Je, benki za Kiislamu hufanya kazi kulingana na sheria za Kiislamu mjini Tulkarm, na mikoa ya Ukingoni wa Magharibi?

Je, Yafaa Kuweka Pesa Kwenye Hizo Benki? Ama Hizo Benki Ni Majina Tu Ya Kuzibia Kazi Za Riba? Na Hayo Tutahakikisha Vipi?

**Jibu:**

Wa Alaikum Salaam wa Rahmatullahi wa Barakatuh,

Kwanza: Tulishawahi kujibu mfano wa hili swali zaidi ya mara moja. Mnamo 20/8/2010, na 5/3/2011… na nitarudia yaliyo lazima kuhusiana na swali lako kutokana na hayo majibu:

[ Kwa hakika, mikataba katika Uislamu sio ya kutatiana, wala sio kwamba haijulikani bali ni mepesi na inajulikana, na imebainishwa katika sheria kwa uwazi kabisa:

1- Muuzaji wa bidhaa yoyote, anapaswa awe anaimiliki, kisha aionyeshe kwa ajili ya kuuza, na mnunuaji naye aione, halafu akiikubali basi mkataba umetimia, na kama si hivyo basi mwenye bidhaa abaki na bidhaa yake. Na haiswihi na haifai katika Uislamu, mtu kuuza bidhaa isiyoimilikiwa na muuzaji. Na miongoni mwa dalili juu ya hilo:

Imepokewa kutoka kwa Hakim bin Hizam akisema:

**قُلْتُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ يَأْتِينِي الرَّجُلُ يَسْأَلُنِي الْبَيْعَ لَيْسَ عِنْدِي مَا أَبِيعُهُ مِنْهُ، ثُمَّ» أَبِيعُهُ مِنْ السُّوقِ«**

**فَقَالَ: «لَا تَبِعْ مَا لَيْسَ عِنْدَكَ»**

Nilisema: **"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, huwa najiwa na mtu akitaka nimuuzie kitu hali ya kuwa sina cha kumuuzia. Kisha namnunua kutoka sokoni. Akasema: usiuze kitu usicho kuwa nacho"** (Imepokewa na Ahmad).

Na imepokewa kutoka kwa Amr bin Shuaib, kutoka kwa babake, kutoka kwa babu yake, amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw):

**«لَا يَحِلُّ سَلَفٌ وَبَيْعٌ، وَلَا شَرْطَانِ فِي بَيْعٍ، وَلَا رِبْحُ مَا لَمْ تَضْمَنْ، وَلَا بَيْعُ مَا لَيْسَ عِنْدَكَ»**

**“Si halali mauzo ya mbeleni (salaf) na mauzo ya hapo kwa hapo (ba'i), wala (si halali) sharti mbili ndani ya mkataba mmoja wa mauzo. Wala (si halali) faida ya ambacho hujakidhamini. Wala (si halali) kuuza kitu usichokuwa nacho”** (Imepokewa na Abu Daud).

2- Na mfano wa hayo, ni akiwa Khalifah atataka kuwagawia watu mali ya Ummah, au kuwagawia chakula kutokana na mali ya serikali, na kila mmoja akajua fungu lake, hapo haifai kwake kuuza funga lake kwa kutanguliza kabla ya kulipokea kutoka kwa serikali.

Na hiyo ndio hali waliyokuwa nayo Maswahaba wa

*Endelea... UK 11*


Email: info@uqab.or.ke

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (saw).

Imepokewa na Malik, kutoka kwa Naafi, kwamba Hakim bin Hizam aliuza chakula ambacho alikitoa Umar ibn Khatwab na kuwapa watu kabla ya (Hakim) kukipokea. Hilo likamfikia Umar ibn Khatwab akamkosoa, na akamwambia: "Usiuze chakula ulichonunua hadi ukipokee".

Na amepokea tena Malik kwamba ilimfikia kuwa misaada kutokana na chakula cha huko Jaar kilitoka kwa ajili ya watu, zama za Marwaan ibn al-Hakam. Watu wakaanza kuuziana hiyo misaada kabla hawajaipokea. Akaingia Zaid bin Thaabit na mtu mwengine kati ya Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) wakaingia kwa Marwaan ibn al-Hakam wakamwambia: "Ewe Marwaan wahalalisha kuuza riba?! Akajibu: "Najikinga kwa Mwenyezi Mungu (nimehalalisha) kivipi?" Wakasema: "Hii misaada, watu wanauziana hata kabla hawajaipokea! Basi, Marwaan akatuma walinzi waifuate na kuwanyang`anya watu mikononi, na kuwarudishia wenyewe".

3- Lakini imedhihiri katika miji ya Waislamu taasisi zinazofanyia hila sheria na kujiita "za Kiislamu". Mfano benki zinazoitwa "za Kiislamu", zinaamiliana kwa riba, lakini sio kwa njia za riba kama zinavyofanya benki zingine bali zinafuata njia zingine zilizoharamishwa:

a- Pindi unapoenda kwa benki za kawaida ukitaka mkopo, basi benki itakupa mkopo kwa faida maalum ya riba. Na unapoenda kwa benki inayoitwa "ya Kiislamu" na ukataka mkopo, basi haitokupa bila ya ziada, kwa sababu hiyo ni benki wala sio taasisi inayosaidia watu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Nayo yataka ziada, lakini sio kwa uwazi kama zinavyofanya benki za kawaida, kwa kuwa jina lake ni la Kiislamu! Kwa hiyo haitaki kuamiliana kwa riba iliyo haramu, uharamu ambao unajulikana na hata watu wa kawaida. Lakini itakwambia: kwa nini wataka mkopo? Utasema: ili ninunue gari, au bidhaa fulani… na similiki thamani yake. Benki itakwambia: vizuri! sisi tutakununulia, na tutalipa thamani yake taslimu, na tutakuuzia kwa malipo ya polepole kwa ziada fulani… na itapitisha makubaliano nawe kabla ya benki kununua yaani, mauzo kati ya benki na wewe kulipa polepole yamepitishwa na mkataba umetimia na tayari imekuwa lazima hata ya benki kununua bidhaa. Hivyo basi unalazimika kuichukua hiyo bidhaa baada ya benki kununua! Ikiwa na maana, mkataba wa mauzo umepita kabla ya benki kumiliki bidhaa. Wewe hukuinunua baada ya benki kuimilki na kukuonyesha ili ukubali au ukatae, bali hapa huwezi kukataa kwa sababu, kimsingi benki ilikununulia wewe na wala si yao. Hivyo, hii ni kuuza usichokimiliki, na hilo halifai kisheria…lau hiyo benki ina mahala pa maonyesho ya magari ambayo wanayamiliki, na wanayaonyesha kwa watu na kuwauzia watakao kwa malipo ya polepole, basi hayo mauzo yangekuwa sahihi. Lakini, benki sio mfanyibiashara kwa maana inayojulikana bali ni benki inayotaka faida kwa mali wanazotoa. Sasa badala ya wao kuchukua ziada ya riba isiyoendana na jina lake la kuwa benki ya "Kiislamu" wanaipata hiyo riba na zaidi yake kupitia muamala usiokuwa wa kisheria, ambao ni: kuuza usichomiliki, ambao ni muamala haramu katika Uislamu!.

b- Wao huita ni "murabaha" lakini sio hivyo kwa sababu, murabaha kisheria: ni uwe wamiliki bidhaa, na uionyeshe kwa ajili ya kuuza, aje anayetaka kununua na muelewane bei, wamuambia nipe faida kadhaa juu ya bei niliyonunua nayo hii bidhaa, basi naye akubali, baada ya kumjulisha bei uliyogharamika kununua nayo hiyo bidhaa, naye pia apate utulivu kwa hilo. Halafu akulipe hiyo bei na faida mliyokubaliana. Na kama unavyoona, hapa muuzaji anamiliki bidhaa pale alipoionyesha kwa mnunuzi. Na ni wazi hivi sivyo yanavyoamiliana mabenki yaitwayo ya Kiislamu ama taasisi zinazofanana nayo!.

c- Wakati mwengine huita ni "ahadi" wala si "mauzo". Na hii pia ni "mughalatwa" (ujanja tu wa kucheza na maneno) na ni kauli isio sahihi. Kwa sababu, ahadi au kuahidiana hailazimishi, lakini katika kuamiliana na benki yalazimisha. Kwa kuwa makubaliano yamepitishwa hata kabla benki haijamilki bidhaa. Kwa hiyo, mtu hawezi kuiambia benki: sitaki tena kununua, baada ya benki kumiliki gari. Hilo haliwezekani katika kuamiliana na benki, kwa sababu mkataba ushapita kabla ya wao kununua gari, hivyo huwa yalazimisha na sio ahadi. Ama ahadi ya kuuza au kununua: huwa kikawaida hailazimishi.

Hakika ahadi ya kununua hailazimishi bali kinacho lazimisha ni mkataba kwa ijab na qabul tu. Na hapo mkataba umeshakamilika kati ya mtu na benki kabla benki haijailiki gari. Kwa hiyo, kilichotimia kati yao ni: mkataba wa mauzo unaomlazimisha mtu. Hivyo, biashara kivitendo ishamalizika kati ya benki na mtu kabla benki haijamiliki gari. Kwa dalili kwamba benki inapomiliki ile gari basi mtu hawezi tena kukataa kununua, na hilo ni kinyume kabisa na hukmu za kisheria ambazo zimebainisha wazi biashara katika Uislamu.

d- Na mara nyingine huita kwamba ni "kununua" na sio mauzo, na kwamba yule mtu ndiye aliyeamrisha kununua, kwa kuiambia benki: ninunulieni gari... hii nayo pia maneno mengine ya makosa. Kwa sababu, huu muamala kwa sifa hii ni "uwakilishi". Yaani: mtu ndiye ameiwakilisha benki imnunulie gari kwa kiasi fulani cha pesa, naye atailipa benki kiasi fulani kwa sababu ya uwakilishi wao... lakini kinachofanyika si hivyo! Kwa sababu, gari litasajiliwa kwa jina la benki kwa kuwa ndio walionunua gari kutoka kwenye maonyesho ya magari, nayo (benki) yamuuzia mtu kwa malipo ya polepole. Na itabakia imesajiliwa kwa jina la benki hadi pale mtu atakapokamilisha kulipa thamani yake inayoitwa malipo ya polepole. Kwa hiyo, haisajiliwi kwa jina la yule mtu, na benki kuwa muwakilishi wake katika kununua kwa malipo maalumu. Bali hivyo sivyo kabisa... kwa hiyo, hiyo sio "uwakilishi" kwa pande zote. Na lau yule mtu

***Endelea... UK 12***

angekuwa ana uwezo wa kimali na ataka kuiwakilisha benki imnunulie gari kwa malipo kadhaa... angekuwa na huo uwezo asingeiendea benki. Bali angeenda kwa aliye bora na mwenye uzoefu zaidi wa kununua na mwenye gharama hafifu kuliko benki!...

Kwa hiyo, hicho wanachokiita “mauzo” kwa hali hii hakikubaliki.

Na kwa ufupi: huu muamala hauruhusiwi kisheria.

Na kwa hakika nimefurahishwa na maoni ya mmoja wao kuhusiana na benki za Kiislamu aliposema: “Hakika benki za kawaida huvuta mali za watu ambao hawajali kuamiliana kwa riba, na hubakia wale watu wenye kujifunga na dini, ambao hawaamiliani kwa riba, hivyo mali zao hubakia nje ya benki za kawaida. Kwa hiyo, benki zinazoitwa “za Kiislamu” zikawa ndio za kuwinda mali za watu wenye kujifunga na dini, hizi benki zikapatiliza kwa njia za miamala mingine isiyokuwa ya riba inayojulikana uharamu wake hata kwa watu kawaida. Wanazipatiliza mali zao kwa miamala isiyo ya kisheria, lakini inakuwa rahisi kuwakinaisha watu wa kawaida kwamba ni katika sheria. Kama vile: kutafuta jina katika (misamiati ya) kisheria kama neno “murabaha” kwa mfano... nalo ni neno lisilokuwa wazi kama riba, bali huenda wengi katika wajifungao na dini hawalijui na hudhani kua yafaa ] Mwisho wa nukuu.

Pili: Ama swali lako kuhusu kuweka pesa kama amana kwenye hizi benki... tushawahi kujibu swali kama hili mnamo 14/10/2012 na hii ndio kama ilivyo:

[ Kinachopelekea kwenye jambo la haramu pia huwa ni haramu. Ndio hii hutumika kwenye kila kitendo, ni sawa iwe ni kitendo cha mtu binafsi anachofanya mwenyewe kwa upande mmoja, ama kiwe kutoka kwa pande mbili, yaani ... mkataba kati ya mikataba. Tofauti pekee ni kwamba, wakati unapofanya kinachopeleka kwenye haramu basi wewe utawajibikia hiyo haramu. Ama unapokuwa wewe ni sehemu katika mkataba, basi uharamu itakuwa tu kwa ule upande ambao ndio uliotumia njia inayopeleka kwenye haramu. Na ikiwa pande zote zimefuata hiyo njia basi madhambi yatakuwa juu yao wote.

Na wewe kuweka amana, yaani akaunti endelevu (current account) isiyo na faida ya riba kwenye benki, basi utakapokuwa na dhana ya nguvu kwamba benki itatumia pesa zako katika riba, hapo haitofaa kuweka amana (current account) kwenye benki. Ila benki hutafautisha kati ya amana za faida ya riba na zile ambazo ni akaunti endelevu (current account) bila faida ya riba. Ama hiyo ya kwanza ambayo huwekwa amana kwa faida hutumiwa katika riba na hilo halina shaka. Ama ile akaunti endelevu: huenda ikatumika hivyo, ima kutokana na akaunti yako endelevu au kutoka kwa akaunti ya mtu mwengine. Na hilo ni kwa sababu, akaunti endelevu (current account) huwa kuna uwezekano wakati wowote kutolewa pesa pale mwenyewe anapotaka... hivyo basi yafanana zaidi na hali ya kuweka amana kwa mtu muovu. Kwa hiyo, kama utasongeka (lazimika) kufanya hivyo basi haina neno kwako, na atakayepata madhambi ni kwao pindi wakiitumia amana kwa isiyo sawa, maadamu hukujua hilo wala hukuridhia. Ni vivyo hivyo benki, kama utajua kuwa watatumia akaunti yako endelevu katika riba, basi haitofaa

Na kwa hali ya kawaida, bora zaidi ni usiweke kwenye benki au kwa mtu muovu.

Lakini yote hayo, ni pale ambapo benki itakuwa imefunga mkataba sahihi. Kama vile ikiwa ni umiliki binafsi, au umiliki wa serikali, au kampuni ya Kiislamu, au kampuni ya hisa iliyofungwa kwa wenyewe... wala sio kampuni ya hisa yenye mkataba batili. La sivyo basi haitaruhusiwa kuamiliana nayo katika hali zote ] Mwisho wa nukuu

**Ndugu Yenu,**

**Atwa Bin Khalil Abu Rashtah**

**9 Dhul Hijja 1442H**

**19/07/2021 M**